# Learning by Ear 2009
# Children's Rights Series
# 03 Children's Parliament

**Maada:** **Bunge la Watoto,Siasa na masual ya Demokrasia yaani**

***Topic**:* *Children's parliament, political and civil engagement for democracy*

**Author:** **Yaya Boudani (Burkina Faso)**

**Editors:** **Sandrine Blanchard / Yann Durand**

**Translator:** **Anne Thomas**

**Kisuaheli:** **Eric Ponda**

| | Women | Men | Age | Language |
|---|---|---|---|---|
| IN/OUTRO | X | | Unimportant | |
| Narrator | | x | Ca. 25 | |
| Nadia | X | | 12 | French |
| Mère | X | | Ca. 35 | French |
| Rachid | | X | Student | French |
| Mamadou Baro | | X | Ca. 45 | French |
| Youssef | | X | Ca. 14 | French |

**LbE Soundtrack**

**INTRO:**

Hujambo na karibu kwa makala yetu ya tatu kwenye mfululizo wa vipindi vya Noa Bongo Jenga Maisha yako kuhusu haki za Watoto.
Leo tunazungumzia suala la Watoto katika siasa. Na moja kwa moja tunafunga safari hadi nchini Burkina Faso, nchi ambayo asilimia 56 ya idadi yake ni watu walio chini ya Umri wa miaka 18, huku asilimia 24 pekee ya watu wazima wakiwa wanajua kusoma na kuandika. Bunge la Watoto limekuwepo nchini humu tangu lilipoanzishwa mnamo mwaka 1998. Jukumu lake kubwa ni kupaza sauti ya mtoto na kuyahimiza mashirika yasiyo ya kiserikali kuhakikisha haki za Mtoto zinalindwa na kuheshimiwa. Yaya Boudani anatujulisha kwa Nadia, ambaye ni mbunge chipukizi katika bunge la watoto la Burkinabe.

**REPORTAGE**

**1. nadia motivation (frz.) 0'24**

"Nilitaka kufahamu vyema masuala ya haki za watoto. Na wakati huo huo kujaribu kuwasaidia watoto wengine. Nilijua nikiwa mbunge nitaweza kuwasaidia kwa namna moja au nyingine na kutafuta

suluhisho kwa matatizo yanayowakabili. Na ndio sababu kubwa ya kutaka kuwa mbunge ili niweze kusaidia katika juhudi za kulinda haki zao. Lakini si watoto wengi wanaofahamu hilo. Tunajukumu kubwa. Na huo ndio msukumo wangu!"

**Narrator:**

Huyu msichana anaitwa Nignan Nadia. Ana umri wa miaka 12 na huenda shuleni mjini Ouagadougou, mji mkuu nchini Burkina Faso. Ari yake ya kutaka kudadisi mambo, ndiyo iliyomwezesha kuchaguliwa katika bunge hili na kuwa makamu wa rais, baada ya kushinda uchaguzi huru na wa haki. Kinyume na ilivyo nchini Ufaransa, wabunge katika bunge la Watoto nchini Burkina, huchaguliwa kupitia kura ya siri.

**2. Nadia élection (frz.) 0'20**

Kwanza kabisa wizara hutuma fomu kwa kila shule, vilabu na hata taasisi zote za watoto. Kisha watoto wawili huchaguliwa kutoka kila shule, klabu au taasisi. Baadaye uchaguzi huandliwa katika kila mkoa, na hatimaye ofisi ya wanachama 10 kufunguliwa katika mikoa hiyo.

**Narrator:**

Si ajabu kumuona Nadia akishikilia wadhifa huu katika bunge hili la watoto. Mamake, Nignan Maïmouna Ouedraogo, anasema kuwa Nadia amekuwa na azma hiyo tangu mwanzoni.

**3. mum : leader (frz.) 0'22**

"Ametaka sana kuwa kiongozi na hadi sasa azma hiyo bado iko. Kila anapokuwa na marafiki zake, wote humfuata yeye--- hata kabla ya kuingia bunge. Ninapokwenda kumchukua shuleni, kila mmoja hutaka kumfuata. Upendo huo baina yake na rafiki zake bado haujafifia licha ya kuingia bungeni. Bado Nadia ni yule yule".

**Narrator:**

Bunge la watoto nchini Burkina Faso linajumuisha watoto wa tabaka mbali mbali. Lina jumla ya wabunge 126 kutoa majimbo yote nchini humo. Sharti kubwa kabisa ni umri. Kwani wabunge wote ni lazima wawe na umri usiozidi miaka 18. Mamadou Baro ni afisa msimamizi wa bunge hili la watoto. Pia husimamia idara ya masuala ya haki za Watoto katika wizara ya huduma za jamii nchini humo

**4. Baro: representativeness (frz.) 0'20**

Kuna watoto ambao hawajaenda shuleni na wengine bado wanasoma. Ngazi zote zinawakilishwa, dini zote pia. Kuna wale wanaorandaranda barabarani ,walemavu, wote wanawakilisha katika bunge hili la watoto.

**Narrator:**

Hali hii ya uwazi inakusudiwa kutoa fursa kwa kila mmoja kutoa maoni, na mijadala inaendeshwa kwa misingi ya Demokrasia. Lakini kama ilivyo katika bunge la taifa, mara nyingine mtafaruku hutokea. Na hapa Nadia anaeleza mbinu wanazotumia kufikia makubaliano.

| **5. Nadia : difference of opinion (frz.)    0'20**<br>Ni kweli hutokea tofauti za kimawazo lakini kila mara tunahakikisha tumekubaliana. Kila mmoja wetu hutoa maoni yake na kisha kutafuta muafaka utakaokubalika na wote. Ofisi hii ni kama familia. Sisi ni kama  ndugu na Dada. Endapo baadhi yetu hawaridhishwi na uamuzi fulani tunajaribu tena kufikiana ili kumridhisha kila mmoja. |
|---|

| **6. Atmo parliament office** |
|---|

**Narrator:**

Vikao vya bunge huanza wakati wa likizo, shule zinapofungwa ili kutoa nafasi ya kila mmoja kuhudhuria. Mijadala huwa mirefu na wabunge hawa watoto huchagua hoja zao wenyewe  wanazotaka kujadilia.

**7. Nadia: topics (frz.) 0'14**

Huzungumzia masuala ya Afya, chakula, miradi mbali na kupanga mikakati ya jinsi tunavyoweza kuwasaidia watoto wengine. Tunataka kuhakikisha kuna usawa wa kijinsia. Haya ndio masuala tunayojadiliana.

**Narrator:**

Wabunge hawa chipukizi hupewa mafunzo ili kuwawezesha kufikia malengo yao. Mafunzo hayo hufanyika katika orofa ya nne ya jengo la wizara ya huduma za jamii ambako maafisa kutoka wizara, shirika la UNICEF na Umoja wa Mataifa hutoa mafunzo kuhusu haki za watoto. Hapa ni Mamadou Baro:

**8. Baro: topics discussed (frz.) 0'41**

Kuna maadili yanayopasa kudumishwa katika sheria kuhusu haki za watoto. Kama vile kumlinda, kumshirikisha na bila kumbagua mtoto yeyote katika masuala ya maendeleo na pia kutilia maanani maoni ya mtoto huyo. Sisi hutoa mafunzo kwa kuzingatia maadili haya na hasa haki ya kila mtoto. Kwa mfano haki ya kwenda shule, afya na kulindwa watoto wanakumbwa na changamoto nyingi. Mfano tatizo la biashara ya kuwauza watoto, unyanyasaji wa kimapenzi, na uhuru wao. Kwa hiyo wanapokutana hujadiliana masuala yanayowaathiri maishani.

**Narrator:**

Baada ya kupata mafunzo na kufahamu majukumu yao, wabunge hawa hukutana na watoto wenzao katika majimbo yao na kujaribu kuzungumza nao na kufahamu vyema matatizo wanayopitia

**9. Atmo moped**

**Narrator:**

Nadia hutumia baiskeli ya Kakake kuzunguka wakati hana kazi nyingi kuwatafuta watoto wanaohitaji msaada. Kwa kawaida huwa haendi mbali kwani kuna watoto chungu nzima wanaofanya kazi au kuomba omba barabarani. Siku moja alikamuona Mtoto mmoja omba omba barabarani, alikwenda kumuona mama wa mtoto huyo:

**10. Nadia : begging child (frz.) 0'42**

Kusema kweli nilisikitika sana na nikamwendea mamake mtoto huyu. Nilizungumza naye kwa kirefu na kumwambia atafute njia nyingine za kumsaidia mwanawe, kwani hapasi kuwa barabarani akiombaomba. Wazazi wanapaswa kuwatunza vyema watoto wao, kuwapa lishe bora, mavazi na kuwapeleka shuleni, Na iwapo mtoto huyo atalazimika kwenda barabarani kuomba, anapasa kuhifadhi nusu ya pato lake na sio pesa zote kuchukuliwa na wazazi wake. Pia nilimwambia kwamba iwapo alikua na matatizo, alipasa kutafuta usaidizi kutoka kwa wizara ya huduma za jamii. Kuna makao

yanayowahudumia kina mama na watoto wao. Alinisikiza kwa makini lakini yaonekana jambo hilo halikumfurahisha. Alishangaa vipi mtoto wa umri wangu anavyoweza kumzungumzia kwa njia hiyo. Lakini alipopata fahamu kuhusu yale niliyokuwa nikimzungumzia aliniahidi kwamba atalifikiria jambo hilo.

**Narrator:**

Wabunge hawa chipukizi pia hupata fursa ya kuhudhuria mikutano na vikao baina ya maafisa wa serikali na makundi ya kutetea haki za watoto. Kwa kuzingatia wadhifa alionao Nadia pia alichaguliwa jaji wa jimbo la Fespaco, jimbo mashuhuri sana kwa utayarishaji wa filamu. Yeye pamoja na wakurugenzi wa filamu za Ki-Afrika alikuwa na jukumu la kuchagua filamu inayozingatia haki za binadamu mbali na maadili mengine ya kijamii.

**11. Nadia : fespaco (frz.) 0'24**

Nilizingatia jinsi filamu hiyo inavyochangia katika kulinda haki za watoto hasa masuala ya afya, masomo, usawa wa kijinsia ,hadhi,usalama na jukumu la wazazi na serikali katika kuwalinda watoto. Kuhakikisha kwamba serikali na wazazi wanatunza watoto.

**Narrator:**

Nadia ana imani kwamba bunge la watoto linaweza kuchangia pakubwa kuwahamasisha zaidi watoto na wazee pia. Lakini kimsingi

bunge hilo bado linakabiliwa na changamoto. Halina vyumba vya kufanyia mikutano, ukosefu wa vikao vya mara kwa mara, vifaa kama vile komputa za kutayarisha ripoti zao. Jambo linalomhuzunisha na kumuibisha makamu huyu wa rais:

**12. Nadia : working equipment 0'16**

Tunahitaji vifaa ili tuweze kufanya vyema kazi yetu. Tunahitaji vyumba vya kufanyia mikutano, tunahitaji kuandaa vikao ili tuweze kukutana mara kwa mara kwani wengi wengi wetu wako sehemu za mbali na ni vigumu kujadiliana masuala muhimu.

**Narrator:**

Nadia ni mtetezi. Alijifunza kwamba maneno matamu humtoa nyoka pangoni na ndio silaha muhimu aliyonayo. Nyumbani sawa na ilivyo shuleni yeye hufanikiwa katika mambo mengi ambayo huonekana kushindikana. Ana ndugu wawili wakubwa lakini wakati mwingi hahitaji msaada wao. Mmoja wao, Rachid, ni mwanafunzi anayesomea sheria mjini Ouagadougou. Anafurahia sana tabia na uwezo wa Dadake

**13. Rachid : no defence (frz.) 0'25**

Yeye hupenda sana kutatua matatizo yake. Sijamuona akitumia nguvu dhidi ya rafiki zake au hata kumtisha mwengine. Wakati mwengine huniambia kuwa amezozana na mwenzake lakini wakasuluhisha mzozo huo kwa amani na hata siku moja hajanitaka kuingilia kati matatizo yake. Huyashughilikia yeye mwenyewe.

**Narrator:**

Anapotoka shule Nadia hutumia wakati wake mwingi kufanya utafiti mtandanoni, kuogolea au kutazama sinema.

**14. Atmo kitchen**

**Narrator:**

Lakini Mamake anapendelea sana Nadia ajifunze upishi kwani bado ana hatua ndefu katika masuala hayo:

**15. Nadia : kitchen (frz.) 0'38**

Kupika Spaghetti naweza (hahaha) na pia mchuzi wa tomato ***attiéké,*** au rojo la njugu..Lakini si mtaalam wa masuala hayo. Napendelea kupika lakini sio vyakula vya Ki-Afrika. Sipendi sana vyakula vya Kiafrika .Mara nyingine husoma vitabu vya mapishi na kujaribu mapishi hayo.

**Narrator:**

Lakini usithubutu kumkasirisha Nadia, ana hasira za haraka sana.Rafiki yake Youssef pia ni mbunge na anafahamu hilo.

| **16. Youssef : reaction (frz.)0'07** |
| --- |
| Mara nyingine hubadilika ghafla hasa tunapozungumzia suala la haki za watoto. Hutufanya tukacheka na kisha baada ya hasira kutulia akarudia hali yake ya kawaida. |

**Narrator:**

Mamake Nadia hakubaliani na jambo hilo:

| **17. Mum : big heart (frz.) 0'06** |
| --- |
| Ana moyo wa huruma sana. Licha ya hasira za haraka. Anapokosewa yeye hujikunyata pembeni na huwa hataki kuzungumza na mtu yeyote. Ndio maana yake. |

**Narrator:**

Wakati atakapokamilisha masomo yake Nadia angependa kuwa wakili au afisa mkuu wa shirika la kutetea haki za Watoto. Lakini kwa sasa anataka kuwania tena kiti cha ubunge ili aendelee kuhudumu katika bunge hilo la watoto kwa kipindi kingine. Lakini hadi wakati

huo, ni wazazi wake watakaojipata chini ya sheria,- sheria za msichana huyu mdogo ambaye amejua haki zake.

**18. maman brought back to order (frz.) 0'09**

Mara nyingi hutuletea sheria hapa nyumbani. Tukifanya jambo fulani anasema tunakiuka haki zake na huenda tukajikuta mbele ya shirika la kutetea haki za watoto UNICEF." (laughter) .

**End music**

**OUTRO :**

Na hadi hapo tunafika mwisho wa kipindi cha leo cha Noa Bongo Jenga maisha yako. Ukipenda kukisikiliza tena kipindi hiki tembelea tovuti yetu www.dw-world.de/lbe Usikose kuungana nasi wakati mwengine kwa makala mengine. Hadi wakati huo kwaheri kwa sasa.